

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



“Mtaa wa Bagara Miyomboni,
S.L.P. 386,
27103 MANYARA,
Barua Pepe: rbcmanyara@pccb.go.tz.
www.pccb.go.tz

MANYARA – NOVEMBA 11, 2020

TAARIFA KWA UMMA

MWENYEKI CCM AREJESHA KIWANJA ALICHOJIMILIKISHA

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Bwagamoyo Wilayani Kiteto Charles Mbaluka amerejesha kiwanja cha Chama Cha Mapinduzi (CCM) alichokuwa amejimilikisha tangu mwaka 2015.

Kitendo cha kiongozi huyo kujimilikisha mali ya umma hutafasiliwa kuwa ni kosa la kutumia madaraka vibaya chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11/2007.

Awali TAKUKURU Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara ilipokea taarifa ikimtuhumu Charles Mbaluka kujimilikisha na kuuza sehemu ya Kiwanja cha CCM kata ya Bwagamoyo kilichotolewa na Serikali ya Kijiji cha Bwagamoyo tangu mwaka 2013 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya chama katika kata hiyo.

Uchunguzi uliofanyika umethibitisha kuwa Chama Cha Mapinduzi mwaka 2013 kilipewa Kiwanja katika Mtaa wa Msente chenye ukubwa wa **930.776m³** na serikali ya Kijiji cha Bwagamoyo

Uchunguzi zaidi ulibaini kuwa Mwaka 2015 mwenyekiti huyo kwa kuvunja maadili ya utumishi wa umma na chama chake cha CCM alijimilikisha sehemu ya eneo la Kiwanja hicho, akalitumia kwa kujenga nyumba yake na kuuza kipande kingine cha eneo hilo kwa Tshs.700,000/=.

Katika uchunguzi huo Mtuhumiwa alikiri kujimilikisha kinyume cha sheria hivyo kwa niaba ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa naomba Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya Kanari Patrick Songea nikukabidha kiwanja hiki ili ukirejeshe kwa viongozi wa (CCM) Kata ya Bwagamoyo ili kitumike kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Rai yetu kwa CCM kuchukua hatua kali za kinidhamu dhidi ya Charles Mbuluka ambaye pamoja na kitendo hicho cha kukihujumu chama bado ni mwenyekiti wa chama wa kata hiyo.

Ni ushauri wetu kwa Baraza la Wadhamini wa Chama Cha Mapinduzi kuzitambua mali za chama kote Mkoani Manyara vikiwemo viwanja na kuhakikisha vinakuwa na hati miliki ili kuziepusha mali hizo kuporwa na baadhi ya viongozi wa chama wasio wadhilifu

Imetolewa na

**HOLLE J. MAKUNGU
MKUU WA TAKUKURU (M)
MANYARA**